



**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA**

**SHULE YA SEKONDARI VUDOI**

**S.L.P 157**

Barua pepe [Vudoisekondari@gmail.com](mailto:Vudoisekondari@gmail.com)

**10/12/2020**

Unapojibu tafadhali taja,  
**Kumb. Na. VSS/K.2018/VOL.I/IV**  
**Simu Na. 0687 786992/0713 566959**  
**0759379856/0719180369**

**JINA LA MWANAFUNZI:** .....  
**S. L. P.** ..... **WILAYA** ..... **MKOA WA** .....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI VUDOI WILAYA YA MWANGA MKOA**  
**WA KILIMANJARO MWAKA 2021 KIDATO CHA KWANZA**

**0.0. UTANGULIZI**

Ninayofuraha kukuarifu kwamba, umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021 Shule ya sekondari vudoi ipo umbali wa Km 2 mashariki mwa barabara kuu ya Dar na Arusha karibu na makazi ya polisi Mwangi. Unaweza kushuka stendi kuu ya mabasi Mwangi na ukafika Vudoi bila shida yoyote. Usafiri wa tekisi kutoka mjini kuja Vudoi unapatikana katika kituo cha mabasi cha Mwangi nauli ni Tsh. 4,000/= tu.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni siku ya Alhamisi tarehe **07/01/2021** hivyo unatakiwa kuja na mzazi wako na kutakuwa na kikao cha wazazi na Uongozi wa shule Saa tatu kamili Asubuhi. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **30/01/2021** kama hujafika basi utakuwa umepoteza nafasi hiyo.

Tafadhali soma kwa makini sana maelekezo / maagizo yafuatayo na ukamilishe mahitaji yote yaliyomo katika barua hii ili uweze kupokelewa shuleni na kuanza masomo bila usumbufu wowote.

**VIAMBATANISHO MUHIMU AMBAVYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAVYO/ KUJAZA:**

- ✓ Fomu **A** ya kukubali kufuata sheria zote na masharti yote ya shule na mkataba wa kutoshiriki migomo fujo zozote na makosa ya jinai ya aina yoyote shuleni.
- ✓ Fomu **B** ya mzazi / mlezi ya uthibitisho wa kulipa ada, michango na mahitaji mengine ya shule.
- ✓ Fomu **C** ya siri inayohusu maelezo binafsi ya mwanafunzi.
- ✓ Fomu ya kupimwa afya na Daktari wa Hospitali ya Wilaya / Mkoa / Rufaa au Kituo cha Afya cha serikali tu.
- ✓ Fomu **E** ya usajili wa mwanafunzi (itajazwa shuleni wakati wa kuripoti).
- ✓ Nakala/copy ya cheti cha kuzaliwa .

## [VUDOI SECONDARY SCHOOL] 2021

**1.0. Mahitaji muhimu****A. Sare za shule**

- (a) Sare za shule pamoja na mahitaji binafsi ya mwanafunzi ni jukumu la mzazi hivyo anapaswa kumnunulia mwenyewe. Sare ya shule hii ni suruali mbili kwa wavulana na sketi mbili kwa wasichana aina ya rangi ya kitambaa ni (**DARK BLUE**) inapatikana shuleni. Ili kuepusha kutofautiana kwa rangi na mishono isiyo zingatia inashauriwa kuwa sare zote zishonwe kwa fundi mmoja aliyeteuliwa na uongozi wa shule kwa maelewano kati ya mzazi na fundi. **Fundi huyo atakuwepo siku ya kikao cha wazazi tarehe 07/01/2021**
- (b) Mashati mawili mapya ya mikono mifupi mfuko mkono wa kushoto, mkanda mweusi mwembamba kwa wavulana ( mzazi anunue mwenyewe)
- (c) Viatu vya ngozi visiwe na visigino virefu na vyenye kufunga kwa kamba haturuhusu simple shoes
- (d) Soksi nyeupe kwa wasichana nyeusi kwa wavulana
- (e) Sweta la shule linalofanana na rangi ya suruali/ sketi kwaajili ya nyakati za baridi ( mzazi anunue mwenyewe)
- (f) Rangi ya hijabu ifanane na sare za shule ( mzazi amshonee mwenyewe) Hijabu isiozingatia maadili haita ruhusuwa
- (g) Mkanda mweusi wa ngozi kwa ajili ya kufunga suruali – upana si zaidi ya inchi moja na nusu na usiwe na chuma kipana / kikubwa cha kufungia na kisiwe na picha au mchoro wowote.

**MASHONO: Suruali zishonwe vizuri, ziwe na mifuko miwili mbele isiyo ya kuchimba na mmoja wa nyuma usio wa kubandika, marinda 2 mbele kila upande, ziwe na mkunjo wa chini (turn-up), luksi za mkanda zisiwe pana, suruali zisibane kwa chini wala zisiwe peckos. Ni marufuku kabisa kuvaa suruali inayoshika maungo ya mwili (inayobana). Ukileta itachanwa. Hii ni kwa suruali zote hata za binafsi za kushindia. Mashono ya suruali yazingatie kuwa inavaliwa kiunoni na sio mlegezo kidogo.**

**B. VIFAA VYA MICHEZO**

- i) Sare ya michezo kwa shule hii ni bukta rangi ya bluu na tisheti rangi ya bluu jezi ya timu ya taifa kwa wavulana na wasichana
- ii) Raba za michezo

**C. VIFAA VYA TAALUMA**

- i) Daftari 12 kubwa (counter book three quire) kalamu ya bluu au nyeusi, pensil na rula
- ii) Mkebe wa hesabu
- iii) (English to English) dictionary
- iv) Writing pads 02 ambazo atakuwa anatumia kufanyie mazoezi ya kila wiki (mzazi anunue mwenyewe)
- v) Pia mzazi/mlezi mnunulie mwanao vitabu vya masomo ya sanaa kulingana na uwezo ulionao ( orodha imeambatanishwa)

**D. CHAKULA CHA WANAFUNZI**

Kwa mujibu wa waraka wa Elimu namba tano (5) – 2015 mzazi/mlezi analojukumu la kumpatia mwanae huduma muhimu ya chakula na katika kutekeleza jukumu hili na kwa kuzingatia mazingira yetu wazazi kwenye vikao vya wazazi wote wamekubaliana kugharamia chakula. Hivyo mnashauriwa kuungana na wazazi/walezi wenzenu katika kuwapatia watoto wenu huduma hii muhimu .

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

- i) **RUHUSA:** - Ruhusa ya kutokuwepo shuleni kwa siku moja au zaidi itatolewa na Mkuu wa shule, Makamu wake au Mwalimu aliyekasimiwa madaraka.
- ii) **MWOMBEZI WA RUHUSA:-** Anayekubalika kukuombea ruhusa ni mzazi/mlezi aliyehandikishwa shuleni na sio mtu mwingine yeyote.

## [VUDOI SECONDARY SCHOOL] 2021

- iii) **MIPAKA YA SHULE:-** Ni marufuku kutoka nje ya mipaka ya shule wakati wote wa masomo/shughuli zingine bila idhini ya mwalimu husika.
- iv) **LUGHA RASMI:-** Unatakiwa kutumia lugha ya kiingereza tu mahali popote shuleni. Mawasiliano kati yako na walimu na wanafunzi wenzako yafanyike kwa lugha ya kiingereza.

**UMEME:-** Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kugusa wala kukaribia miundombinu ya umeme mfano: swichi, soketi, taa, swichi kuu wala mita bila sababu za msingi. Tendo la kuwasha taa. Lifanywe mara moja tu sio kubonyeza bonyeza. Nikosa kujiunganishia nyaya za umeme kwa matumizi yoyote yasiyo rasmi, ukikamatwa utafukuzwa shule mara moja. Ukihurumiwa, utaleta roll ya waya 1.5 mm mita 100 pamoja na gharama ya fundi.

### **USAFI BINAFSI:-**

- ✓ Ni lazima mwanafunzi awe msafi na nadhifu wakati wote.
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kufuga ndevu, nywele ndefu wala kusuka kwa namna yoyote ile.
- ✓ Ni marufuku pia kunyoa nywele zote na kubaki na upara. Nywele ziruhusu kijiti cha kiberiti kukaa bila kudondoka.
- ✓ Kucha za miguu na mikono sharti ziwe fupi na zisipakwe rangi yoyote.
- ✓ Sare ya shule ni lazima iwe safi na iliyonyooshwa vizuri. Viatu pia vipakwe rangi yake.
- ✓ **Suruali zitavaliwa kiunoni na sio katikati ya makalio (“kata k”).** Mikanda mipana yenye chuma kubwa sehemu ya kufungia na yenye mapichapicha haikubaliki shuleni.
- ✓ Ni lazima uoge mwili mzima ili kuzuia harufu mbaya.
- ✓ Ni marufuku kujipaka / kujipulizia manukato makali wakati wa darasani.
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa mapambo mfano pete, bangili, hereni, mkufu au kidani cha aina yoyote.
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa viatu vya mchuchumio (Raizoni) wala vya wazi (open shoes wala yeboyebo) wakati wote wa masomo.
- ✓ Nguo za kushindia zisizidi suruali 3 na mashati matatu tu. Mavazi magumu (jeans) hayakubaliki.

### **VIFAA KWA AJILI YA UTUNZAJI WA MAZINGIRA**

Vikabidhiwe shuleni siku ya kuripoti mwanafunzi

- i) Fagio la chelewa la wima 02
- ii) Ndoo kubwa Lt 10 – 01
- iii) Jembe na mpini 01
- iv) Hard broom 01
- v) Cob web 01( ufagio mrefu wa kutolea buibui)
- vi) Panga 01 (kwa wavulana)
- vii) Squizer 01( kwa wasichana)
- viii) Soft broom 01

### **USAFI WA MAZINGIRA**

- Ni wajibu wako kuliweka eneo la shule, majengo na madarasa katika hali ya usafi. Hairuhusiwi kuchora chora wala kuandika katika kuta za majengo ya shule.
- Kila mwanafunzi atapewa eneo la kuhudumia usafi na miti ya kutunza. Ikitokea mti ukafa kwa uzembe, atapaswa kulipa.
- Uchafu na takataka zitupwe mahali panapostahili.
- Ni jukumu la kila mwanafunzi kupendezesha maeneo ya shule yetu ili yavutie.

## [VUDOI SECONDARY SCHOOL] 2021

**2.0. MWENENDO NA TABIA:**

- + Ni marufuku kabisa kwa wanafunzi kuanzisha magenge/vikundi visivyo rasmi shuleni, mfano vya kikabila, vya kidini, vya kimikoa/kikanda, vya kimkakati fulani wa kutisha wanafunzi wengine na kuhukumu. Watakaobainika watafukuzwa shule mara moja.
- + Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvuta sigara, bhangi, kutumia madawa ya kulevya, kunywa pombe, kwenda katika kumbi za starehe mfano disko, baa ama kuonekana maeneo yanayouzwa vileo wakati wote uwapo shuleni au nyumbani kwenu.
- + Ni kosa kutoa matusi au kutumia lugha ya matusi wakati wote ndani na nje ya shule.
- + Ni kosa kubwa kuiba mali ya mtu mwingine ikiwemo mali ya shule, walimu ama ya mwanafunzi mwenzako.
- + Ni muhimu kufahamu mipaka yote ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- + Ni marufuku kwa mwanafunzi kuingia maeneo ya giza ama kificho hapa shuleni au nje ya shule wakati wote.
- + Unatakiwa kuzingatia kwa umakini maandalio ya mchana na jioni (preparations).
- + Ni marufuku kutembelea nyumba za walimu wa watumishi bila ruhusa ya mwl. wa zamu.
- + Ni marufuku kutomasana baina ya wavulana na wavulana, wavulana na wasichana (wowote) ama wenye jinsia moja mahali popote, njiani au maeneo unayoishi.
- + Ni mwiko kabisa mwanafunzi kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanafunzi mwenzake, Mwalimu, Mtumishi asiye Mwalimu au mtu mwingine yeyote.
- + Ni kosa kumdharau, kugombana au kumpiga kiranja au kiongozi wa ngazi yoyote shuleni.
- + Utoro shuleni na utoro wa vipindi vya darasani ni kosa kubwa la kukurejesha nyumbani kwenu.

**ANGALIZO:**

- + Uhusiano kati yenu ni wa kaka na dada na pia baba/mama na mtoto kwa walimu na watumishi wasio walimu. Aidha, kuwepo na mipaka ya mazungumzo na mahusiano (Social distance) kati ya wanafunzi na mwalimu au mtumishi asiyekuwa mwalimu.
- + Lugha za kujirahisi na zisizo na staha haziruhusiwi. Mavazi, mitindo ya mavazi, mitindo ya uvaaji na unyoaji usiyozingatia maadili ya Kitanzania ni marufuku hapa shuleni.

**NB: ZINGATIA HAYA:**

- + **Ni mwiko kuwa na simu ya mkononi au laini ya simu ukikamatwa nayo umejiondoa mwenyewe shule**
- + Mwanafunzi asiyefanya mtihani bila sababu ya msingi atapewa adhabu kali na atagharimia utungaji na usahihishaji wa mtihani mwingine atakaopewa.
- + Kuanzisha magenge/vikundi visivyo rasmi shuleni, mfano vikundi vya kikabila, vya kidini, vya kimkakati fulani wa kutishia wanafunzi wengine na kuhukumu. Watakaobainika watafukuzwa shule mara moja.
- + **Kumiliki simu ya mkononi au laini ya simu au kupatikana na vifaa vya kuchajia simu.**

**[VUDOI SECONDARY SCHOOL] 2021**

**MAKOSA MAKUBWA YA KUMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI:**

- ✚ Wizi, Uasherati, Kuoja au kuolewa. Ulevi wa aina yoyote kupiga au kupigana, kudharau uongozi halali wa serikali ya wanafunzi, kuanzisha au kushiriki mgomo shuleni, kuharibu kwa makusudi mali ya umma, kuharibu au kudharau Bendera ya Taifa, picha za Viongozi wa Kitaifa, Wimbo wa Taifa na kuharibu Fedha za Taifa(Alama za taifa).
- ✚ Mwanafunzi akisababisha au kupata mimba ataachishwa masomo na kushtakiwa kwa mujibu wa sheria.
- ✚ Kukataa adhabu ni kosa kubwa la kupelekea kufukuzwa shule.

**3.0. UMUHIMU WA KUJISOMEA:** Ni muhimu sana kwa mwanafunzi kujenga tabia ya kujisomea na kufanya maandalizi ya siku inayofuata. Inasisitizwa mwanafunzi kutenga muda wa kutosha kujisomea na kufanya kazi alizopewa na mwalimu wake shuleni.

**4.0. JIVUNIE SHULE YAKO:** Kila mwanafunzi aipende na ajivunie shule yake. Aidha, kila mzazi / mlezi aipende na ajivunie shule anayosoma mtoto wake na antimize mahitaji yake ili awawezeshe walimu na watumishi wengine kutoa elimu bora.

**5.0. MZAZI/MLEZI KUMBUKA NA KUZINGATIA:**

Kila mzazi / mlezi azingatia kuwa jukumu la kumsomesha mtoto wake ni la kwake mwenyewe. Itakuwa haina maana yoyote kumleta mtoto wako katika shule hii na kumtelekeza bila kumpatia mahitaji yake ya msingi na mwisho wa yote utegemea miujiza itokee mwanao afanye vizuri. Inawezekana, timiza wajibu wako sasa.

**6.0. TANBIHI: Pamoja na maagizo haya, tafadhali tekeleza yafuatayo:-**

Tuandikie tujulishe rasmi kukubali kufuata sheria za shule hii kwa kujaza fomu A iliyoambatanishwa na uirejeshe siku ya kuripoti shuleni.

- Jaza fomu **B** inayohusu uthibitisho wa kulipa ada na uirejeshe siku ya kuripoti.
- Jaza fomu **C** inayohusu maelezo binafsi ya mwanafunzi (Fomu ya siri) na uiwasilishe kwa mkuu wa shule siku ya kuripoti.
- Jaza fomu **D** (ripoti ya Daktari) – ijazwe na Hospitali yenye hadhi ya Kituo cha afya , wilaya au mkoa na sio zahanati na pia iletwe siku ya kuripoti.
- Fomu **E** inahusu usajili - Itajazwa na kila mmoja baada ya kuonyesha mahitaji na michango yote wakati wa kuripoti shuleni.
- Hakikisha unaandika jina lako kwa kudarizi katika sare zote, shuka, track suit na blanketi.

**MWISHO:** Kwa niaba ya bodi ya shule walimu na wafanyakazi wote, nakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na shule yetu. Na Imani yetu kuwa utaitumia vizuri nafasi hii uliyotunukiwa na Taifa.

**KARIBU SANA VUDOI SEKONDARI**

.....  
**O.M.MBELENJE**  
**MKUU WA SHULE**

## [VUDOI SECONDARY SCHOOL] 2021 FOMU A

**HATI YA MAKUBALIANO/MKATABA  
KUKUBALI KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE**

**A. HABARI ZA WAZAZI/WALEZI NA WANAFUNZI****SEHEMU A: ( HABARI ZA MWANAFUNZI)**

1. Jina kamili (kama kwenye mtihani) .....
2. Tarehe ya kuzaliwa.....Dini.....
3. Mahali na wilaya alipozaliwa.....
4. Shule uliomaliza darasa la saba.....  
Mwaka uliomaliza.....
5. Kidato chako unachokuja kuingia hapa shule ya sekondari Vudoi .....
6. Matatizo ya afya uliyonayo mwanafunzi.....

Picha ya  
mwanafunzi

**B. HATARI ZA MAZAZI/MLEZI**

- i) Jina kamili la mzazi/mlezi .....
- ii) Mahali anapoishi.....
- iii) Wadhifa/kazi yake.....
- iv) Mahali anapofanya kazi.....
- v) Namba za simu za mzazi/mlezi.....
- vi) Namba za simu za mtu mwingine wa karibu.....

Picha ya  
mzazi/mlezi

**C. AHADI YA UTII/TABIA NJEMA**

Mimi.....(Jina kamili la mwanafunzi) wa kidato cha....naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu na mbele ya mkuu wa shule.

- a) Kwamba nitafuata sheria na kanuni za shule pamoja na maelekezo yote halali yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule
- b) Kwamba nitatii
- c) Kwamba sitatoka nje ya mipaka ya shule labda tu kwa ruhusa maalumu kwa mwalimu wa zamu, mwalimu mlezi, makamu mkuu wa shule au mkuu wa shule mwenyewe
- d) Kwamba sitamiliki simu ya mkononi wala laini ya simu wala kifaa chochote kinachotumia umeme.
- e) Kwamba kama nitashindwa kufuata au kuzingatia maadili mema nipewayo na walezi wangu shuleni hatua kali zichuliwe dhidi yangu ambayo ni pamoja na kuachishwa masomo.

**D. AHADI YA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO/FUJO/KOSA LA JINAI**

Mimi.....(jina kamili la mwanafunzi) wa kidato cha .....mwaka.....natambua vema wajibu wangu kwa Taifa kama mwanafunzi kwa hiyo naahidi kutojihusisha na mgomo, fujo au ushawishi wa aina yoyote wa kusababisha mgomo au makusanyiko katika shule. Aidha naahidi kuwa sitashiriki katika makosa yote ya jinai nanikibainika kuchochea ama kushiriki mgomo au jina yoyote basi nifukuzwe shule mara moja.

**AHADI HII NIMETOA LEO .....**(Siku) **Tarehe .....**Mwaka.....

**JINA LA MZAZI/MLEZI**

**SAHIHI YA MZAZI / MLEZI**

**JINA LA MWANAFUNZI**

**SAHIHI YA MWANAFUNZI**

**JINA LA M/KITI WA KIJIJI/MTAA AU MTENDAJI WA KATA**

**TAREHE.....**

**SAHIHI.....**

.....  
**O.M.MBELENJE  
MKUU WA SHULE**

## [VUDOI SECONDARY SCHOOL] 2021

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
SHULE YA SEKONDARI VUDOI  
S.L.P 157  
MWANGA  
SIMU. 0687 786992**

**FOMU B**

**FOMU YA UTHIBITISHO WA KUMPATIA MWANAO MAHITAJI YA SHULE KWA WAKATI**

Mimi.....mzazi/mlezi wa  
mwanafunzi.....(Jina la mwanafunzi) nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu  
aliyechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Vudoi ni mzaliwa wa kijiji cha.....kata ya  
.....wilaya ya.....mkoa wa .....Nitampatia mwanangu  
mahitaji yote muhimu ya shule mwanzo wa muhula bila kusumbua uongozi wa shule.

.....  
**JINA LA MZAZI/MLEZI**  
**TAREHE.....**

.....  
**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI**

.....  
**MTENDAJI/ MWENYEKITI WA KIJIKI**

.....  
**MHURI WA KA KIJIKI**

.....  
**MTENDAJI KATA**  
**TAREHE .....**

.....  
**MHURI WA KATA**

**TANBIHI**

Endapo una mfadhili wa kumlipia mwanao, uthibitisha hapa chini kwa maandishi sahihi na mhuri jinsi atakavyolipa na malipo hayo yafanyike kabla ya mwezi machi 2019 ili kurahisisha utendaji

**MFADHILI**

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

## [VUDOI SECONDARY SCHOOL] 2021

## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

JAZA FOMU HII KWA UKWELI. HII NI SIRI KATI YAKO NA MKUU WA SHULE TU

## 1. ANDIKA MAJINA KAMILI

- i) Majina yako halisi.....
- ii) Majina yako ya nyumbani.....

	JINA	BABA	UKOO	UMRI	Tarehe ya kuzaliwa
LAKO					
BABA					
MAMA					

## 2. NYUMBANI

Kiji/Mtaa.....Kata.....

Tarafa.....Mkoa.....

## 3. ANUANI YA NYUMBA

.....

4. Kukiwa na tatizo taarifa ipelekwe kwa nani..... Uhusiano na wewe.....
- Anafanya kazi gani na wapi?.....

## 5. Wazazi na ndugu.

Baba yuko hai?.....Mama yuko hai?.....

Baba anao watoto wangapi?.....wavulana.....wasichana.....

Baba ana wake wangapi?.....wewe ni mtoto wake wa ngapi.....

Mko wa ngapi kwa mama yako?.....wewe ni mtoto wangapi kwa mama.....

6. Dini yako .....Dhehebu.....

## UNAOWATEGEMEA

7. (a) Unaishi na nani na wapi?.....
- (b) Nani anayekupa mahitaji ya shule? .....

TOA SABABU KAMA SIO MZAZI .....

.....



[VUDOI SECONDARY SCHOOL] 2021 FORM D

THE PRESIDENT’S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
VUDOI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 157 MWANGA
MOB. 0713 566954

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To.The Medical Officer

.....
.....
.....

Please examine.....(student) as to his fitness to pursue secondary Education without any problems.

.....
HEAD MASTER

History: Mental illness? \*Yes/No .....Asthma and other allergies?
Yes/No. Stool.....
Urine: Sugar.....Protein.....Cells.....
Blood: ESR.....FBT-WBC Total.....Differential.....
.....Hb.....gm/dl BS.....
Vision acuity: Right eye.....Left eye.....
Chest: Clinical.....
Chest X – ray.....

Any physical/mental disability \*Yes/No if yes please describe in simple terms
.....

I have examined the above named student and found that he/she is \*FIT/UNFIT to pursue secondary school education.

Name of the medical inchange.....Signature .....

Date.....